**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA**

Kumb Na.EA.89/286/01B/11 29/05/2025

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara amepokea kibali kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kilichotoa idhini ya utekelezaji wa nafasi za Ajira Mpya katika ikama ya mwaka wa fedha 2024/2025 chenye Kumb. Na. **FA. 97/228/01/A/25** cha tarehe **29 April, 2025**. Hivyo anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa kutuma maombi ya kazi katika nafasi zifuatazo:-

## 1.0. MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA II – NAFASI 04

### 1.1. SIFA ZA MUOMBAJI

Awe na Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au cha Sita (Form VI) na amehitimu Stashahada/Diploma ya Uhazili au Cheti cha NTA Level 6 ya Uhazili. Aidha awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa Dakika Moja na kupata program za kompyuta za ofisi kama vile:- Word, Excel, Power Point, Internet, E-mail, na Publisher kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.2. KAZI NA MAJUKUMU

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida na siri,
ii. Kupokea wageni na kuwasilisha shida zao na kuwaelekeza wanapoweza kusaidiwa;
iii. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi;
iv. Kupokea majalada na kusambaza kwa maofisa walio katika Divisheni, Vitengo na Sehemu zinazohusika;
v. Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika;
vi. Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali; na
vii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya ofisi.

### 1.3. NGAZI YA MSHAHARA.

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali - **TGS C 1.**

## .0. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II - NAFASI 04

### 2.1 SIFA ZA KUAJIRIWA- MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II

Mwombaji anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

a) Mwenye elimu ya Kidato cha Nne (K.IV) au sita (K.VI).
b) Awe na cheti cha Stashahada (Diploma) (NTA LEVEL 6) cha utunzaji wa kumbukumbu katika fani ya Utunzaji wa Kumbukumbu kutoka vyuo vinavyotambuliwa na serikali, na mwenye ujuzi wa Kompyuta.

### 2.2 KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA LA II:

Mwombaji atakayefaulu/ atakayekidhi vigezo na kuajiriwa atatekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Kuorodhesha barua zinazoingia masijala kwenye Rejista (Incoming Correspondence Register)
ii. Kuorodhesha barua zinazotoka nje ya taasisi (Outgoing Correspondence Register).
iii. Kusambaza majalada kwa Watendaji (Action Officers).
iv. Kupokea Majalada kutoka kwa Watendaji (Action Officers).
v. Kupokea majalada yanayorudi kutoka kwa Watendaji.
vi. Kurudisha masijala kwenye Shabaka/ Kabati la Masijala (Racks/Filling Cabinets) au mahala pengine yanapohifadhiwa.
vii. Kufuatilia mzunguko wa majalada ndani ya Taasisi (File Tracking).

2.3 **Mshahara** – Ngazi ya mshahara itakuwa ni **TGS/C/1**

## 3.0. MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI.

- Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri usiozidi miaka 45 na umri usiopungua miaka 18,
- Waombaji waambatanishe Cheti cha Kuzaliwa,
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye Anuani, Namba za Simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wa kuaminika,
- Waombaji wote waweke nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya Kidato cha Nne na Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika kwenye ***Ajira Portal,***
- ***Testimonials "Provision Results", "Statement of Results" Hati ya Matokeo ya Kidato cha Nne na Sita HAVIKUBALIKI,***
- Waombaji wote waweke picha mbili *"Passport Size"* ya hivi karibuni katika ukurasa wa *Ajira Portal*,

- Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe vyeti vyao vinahakikiwa na kuthibitishwa na mamlaka husika yaani TCU, NECTA na NACTE,
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi,
- Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka wenye Kumb. Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010,
- Uwasilishwaji taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria,
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **12 Juni, 2025,**

**MUHIMU**: Kumbuka kuambatisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na anuani. Barua ya maombi ielekezwe kwa: -

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya ya Ngara,**
**S.L.P 30,**
**NGARA.**

i. Maombi yote yatumwe kwa njia ya mfumo wa kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; https://portal.ajira.go.tz/ (Anuani hii pia inapatikana kwenye tovuti ya Sektretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu iliyoandikwa 'Recruitment Portal').

ii. Maombi yatakayo wasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFANYIWA KAZI**.

Imetolewa na;

Solomon .O. Kimilike
**MKURUGENZI MTENDAJI**

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NGARA